

MAMLAKA YA USIMAMIZI WA WANYAMAPORI TANZANIA



MATUKIO YA ASKARI WA PORI TENGEFU KILOMBERO KUVAMIWA NA KUSHAMBULIWA NA WATU KWA LENGU LA KUPORA MIFUGO ILIYOKAMATWA NDANI YA HIFADHI

Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania (TAWA) imepokea kwa masikitiko makubwa taarifa za matukio mawili (2) ya Askari wa Uhifadhi kuvamiwa na kushambuliwa na vikundi vya watu wanaoashiria kuwa wafugaji kwa lengo la kupora mifugo iliyokamatwa. Matukio hayo yalitokea tarehe 17 Novemba 2022 katika Wilaya za Malinyi na Ulanga ndani ya Pori Tengefu Kilombero ambalo ni chanzo muhimu cha maji yanayotegemewa kwa ajili ya kuzalisha umeme katika bwawa la Mwalimu Nyerere.

Tukio la kwanza lililotokea tarehe 17 Novemba 2022 majira ya saa saba mchana ambapo askari wakiwa maeneo ya Mto Furuu ndani ya Pori Tengefu Kilombero, walivamiwa na kundi la watu takriban 60 wakiwa na silaha za jadi ikiwemo fimbo, sime, mikuki na mapanga kwa lengo la kupora ng'ombe 150 waliokuwa wanashikiliwa. Askari walifanikiwa kudhibiti uporaji huo, huku mtu mmoja akijeruhiwa kwa risasi mguuni. Mtuhumiwa huyo alifikishwa hospitali kupatiwa matibabu na bado yupo chini ya ulinzi. Tukio hili liliripotiwa Kituo cha Polisi Malinyi.

Tukio la pili lilitokea tarehe 17 Novemba 2022 majira ya saa 10 jioni katika eneo la Senga Wilaya ya Ulanga ndani ya Pori Tengefu Kilombero ambapo takriban watu 40 wakiwa na silaha za jadi walivamia na kushambulia askari. Katika kujihami, askari walifyatua risasi hewani kwa lengo la kuwatahadharisha na kuwatawanya watu hao ambao waliendelea kuwashambulia na kutokea mapigano kati yao. Aidha, watu hao walifanikiwa kupora mifugo takriban 200 iliyokuwa inashikiliwa na kujeruhi askari wawili. Askari wa kwanza alijeruhiwa kichwani na kitu chenye ncha kali ambapo alivuja damu nyingi na kupoteza fahamu, alipozinduka alijikuta akiwa hana silaha. Askari wa pili alijeruhiwa kichwani na mguuni. Wote walipelekwa hospitali na kupatiwa matibabu.

Ukaguzi uliofanyika eneo la tukio kwa kushirikisha Jeshi la Polisi uliwezesha kupatikana kwa silaha iliyopotea na kubaini miili ya watu watatu ambayo ilifanyiwa uchunguzi na Jeshi la Polisi na Daktari kisha kukabidhiwa kwa ndugu zao kwa ajili ya mazishi. TAWA inashirikiana na Jeshi la Polisi kuhakikisha inawabaini na kuchukua hatua za kisheria kwa watu wote waliohusika na vurugu hizo. Aidha, TAWA inawaomba wananchi kuwa watulivu kwa kuwa Jeshi la Polisi linaendelea na uchunguzi wa matukio hayo.

Vilevile, TAWA inatoa rai kwa wananchi kutoa ushirikiano katika ulinzi wa maeneo ya hifadhi na vyanzo vya maji. Aidha, TAWA inawataka wananchi kufahamu kwamba kuingia ndani ya maeneo ya hifadhi na kufanya shughuli za kibinadamu bila kibali ni kosa la jinai na inaomba wananchi kuheshimu sheria ili kuepuka mitafaruku isiyokuwa ya lazima.

Imetolewa na Idara ya Uhusiano kwa Umma-TAWA